SWAHILI FORUM 22 (2015): 104-118

ISHARA NA UASHIRIAJI KAMA NYENZO YA MTINDO, MAANA NA KIWAKILISHI CHA ITIKADI KATIKA RIWAYA YA *NYUSO ZA MWANAMKE*

MUKHATA CHRISPINUS WANYONYI

This article analyses symbols and symbolism as stylistic devices of communicating meaning and as a technique of characterisation and theme development in *Nyuso za Mwanamke* (The Faces of a Woman, 2010) written by Said Ahmed Mohamed. I analysed three types of symbols which are natural symbols, conventional symbols and literary symbols following Frye et al. (1985). This study aims at showing how symbols are used in literary works to communicate meaning and the ideology of the society depicted in the text. Symbols also help to build the theme, the plot and adding aesthetic value in literary texts.

Makala haya yanachanganua ishara na uashiriaji kama mbinu ya kimtindo ya kuwasilisha maana na kukuza uhusika na maudhui katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) ya Said Ahmed Mohamed. Nimechanganua aina tatu za ishara ambazo ni ishara bia, ishara za kaida na ishara za kifasihi kama zinavyoainishwa na Frye na wenzake (1985). Lengo kuu ni kuchanganua na kubainisha jinsi ishara zinavyowasilisha maana na itikadi za jamii katika matini husika. Ishara hizi pia husaidia kukuza maudhui, ploti na kuongeza ujumi katika matini za kifasihi.

Utangulizi

Makala haya yanalenga kuchanganua dhana ya ishara na uashiriaji kama mbinu ya kimtindo katika riwaya ya Nyuzo za Mwanamke (2010). Riwaya hii ni riwaya ya nane ya Said Ahmed Mohamed, mwandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili ya kisasa. *Nyuso za Mwanamke* (*NM*) ni riwaya ya kisaikolojia kwa sababu imeweka msisitizo mkubwa kwenye fikira na hisia za ndani za wahusika. Aina hii ya riwaya mara nyingi hujihusisha na mawazo ya mhusika anayesumbuka kimawazo na kihisia (Wamitila 2003: 181). Hali ya kisaikolojia ya mhusika wa riwaya ya aina hii hudhihirishwa na matukio ya kinjozi na ishara.

Riwaya hii inazungumzia masuala ya mitagusano ya kimaadili, kiuchumi, kijamii na kisiasa katika jamii ya Kisiwa cha Unguja. Kazi hii inazungumzia maisha ya Nana, msichana anayejikuta katika mivutano ya kifamilia, kijamii, kitamaduni, kidini na kinafsi; anayeathirika na kubebeshwa makosa yaliyofanywa na wazazi wake, hasa baba yake. Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* inatudokezea “nyuso," yaani taswira mbalimbali walizo nazo wanawake katika harakati za kudhulumiwa na kudhalilishwa na mfumo wa ubabedume. Inamsawiri mwanamke wa Kiafrika katika kipindi hiki cha utandawazi anayejaribu kujikwamua kutokana na minyororo ya kitamaduni.

ISHARA NA UASHIRIAJI KAMA NYENZO YA MTINDO, MAANA NA KIWAKILISHI CHA ITIKADI KATIKA RIWAYA YA *NYUSO ZA MWANAMKE*

Ufafanuzi wa dhana ya ishara

Ishara ni kitu kinachosimamia kitu kingine kinachohusiana nacho. Kulingana na Frye na wenzake (1985: 451) “ishara ni kiashirii na kile inachosimamia ni kiashiriwa.” Kwa mfano, msalaba ni ishara ya Ukristo na rangi nyeusi kwa Wazungu ni ishara ya kuomboleza. Kwa maoni yao ishara huwakilisha kifikira maana na hali ya kitu kinachoashiriwa. Kwa mujibu wa Perrine (2014: 171) “ishara ya kifasihi ni kitu kilicho na maana zaidi ya kitu hicho. Yaani, ishara ni kitu, mtu, hali, tukio au kitu chochote kile kilicho na maana ya kawaida lakini kinaashiria au kinawakilisha maana nyingine zaidi.” Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa ishara si kitu pekee bali pia hurejelea tukio, hali au mtu anayeweza kutumiwa kudokeza maana kiishara. Kama anavyoongeza Snowden (2006: 85) ishara hujumlisha vitu hai na visohai pamoja na vitu dhahania. Anadai maksai, mtu, simba na tai katika dini ya Kikristo ni viumbe vinavyoashiria wahubiri wanne. Mkuki kama kitu kisohai kinaashiria sehemu ya uume ilhali giza ni ishara ya uovu. Kitu, hali au tukio linalotumiwa kiishara katika matini za kifasihi huwa na maana iliyo zaidi ya maana ya kawaida na inayohusiana na kiashirii. Kwa maana hii basi nitaiangalia ishara kama kitu, hali, tukio, neno, mtu au mandhari yanayowakilisha maana ya ziada ya kiashirii na yenye mahusiano na kiashirii hicho. Maana hii ndiyo nitakayoichukulia kama fasili ya ishara.

Ishara kama mbinu ya mtindo inayotumika kama nyenzo ya kuwasilisha maana, huweza kuwa tata kubainishwa. Perrine (2014: 172) anadai kuwa ishara katika baadhi ya matini huingizwa katika muktadha wa matini kiasi kwamba inakuwa vigumu kubainika kwa msomaji. Hali hii hutokea sana katika matini zinazokiuka uhalisia ambapo ishara ni nyenzo ya kubeba maana. Katika matini za kihalisia ishara huchukua sehemu muhimu na huwa dhahiri zaidi huhimili ujumbe na kuongeza maana. Kwa maoni yangu matini za kihalisia husawiri matukio kama yalivyo katika maisha ya kila siku na ujumbe huwasilishwa kwa njia ya moja kwa moja. Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ni matini ambayo inakiuka uhalisia kwa vile matukio mengi yamesimuliwa kupitia ndoto, uzungumzinafsi ndani na mkondo wa ung.amuzi.

Katika matini nyingi za kifasihi ishara huweza kuwa na maana zaidi ya moja. Kutokana na mawazo ya Perrine, ishara ni kama kitu cha thamani chenye rangi nyingi kinachoweza kudhihirisha rangi mbalimbali kinapowekwa kwenye mwangaza (2014: 174). Maana hizi za ishara hujitokeza kutegemea miktadha ya matumizi. Mawazo haya ya Perrine yanaungwa mkono na Meyer (2002: 179) anayedai kuwa maana za ishara zimekitwa katika mpangilio wa matini na kwa hivyo zinahimiliwa na miktadha ya matumizi yake. Miktadha hii inaweza kuwa ya kidini, kisiasa, kijamii au ya kiuchumi. Kwa mfano, DiYanni (1998: 509) anaeleza kuwa katika muktadha wa kawaida wa kijamii, maji ni ishara ya uhai lakini katika muktadha wa kidini maji yanayojitokeza kama mafuriko ni ishara ya kifo au majaribu. Kwa maana yake maji, yaani mafuriko ni ishara ya tukio baya. Katika muktadha wa kidini maji ni ishara ya uhai, usafi na

tumaini. Nao moto ni ishara ya uharibifu katika muktadha wa kijamii ilhali katika muktadha wa kidini moto ni ishara ya utakaso. Ingawa ishara hutegemea muktadha fulani katika ufasiri wake, inaweza kueleweka kiyakinifu kwa kufahamu dhamira na muktadha wa kijumla wa matini. Kimsingi, ishara hailengi maana mahsusi bali hupendekeza maana inayohusiana na kiashirii.

Ufafanuzi wa dhana ya uashiriaji

Uashiriaji ni mbinu ya kifasihi ambayo ina historia ndefu. Kulingana na Abrahams (1971:170) uashiriaji kama mbinu ya kuwasilisha maana katika matini za kifasihi ilianzia kule Ufaransa katika karne ya 19. Abrahams anasema kuwa mwasisi wa mbinu hii alikuwa Baudelaire katika diwani yake ya mashairi *Les Fleurs du Mal* (1857), yaani "Maua ya Maovu." Watunzi wa mashairi ya Kifaransa wa wakati huo kama Rimbaud, Verlaine, Mallarme na Valery walitumia sana uashiriaji uliohusu matumizi ya ishara za kibinafsi. Katika kipindi hiki uashiriaji kama mkondo wa ushairi uliangaliwa kama mbinu ya kukuza maudhui kwa kujenga uwiano, toni na wizani kitaswira kwa matumizi ya lugha teule. Wakati huu uashiriaji uliangaliwa kama mtindo hasa katika ushairi. Baadaye, uashiriaji kama mbinu ya kifasihi ulienea na kuanza kutumika huko Uingereza na Marekani mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 katika ushairi. Watunzi wa kipindi hiki waliotumia ishara ni kama T. S. Eliot, Arthur Symons, E. E. Cummings na Wallace Stevens. Hii haina maana kuwa uashiriaji ulianza tu katika sehemu hizi za dunia kwa sababu uashiriaji ni mbinu inayojitokeza katika ushairi wa Kiswahili ulioandikwa katika kipindi hiki pia. Kwa mfano, katika Utenzi wa *Al-Inkshafi* (1820) kuna ishara nyingi zilizotumika kama vile mahame na magofu kuashiria kuanguka kwa ufalme wa Pate. Lililo dhahiri katika maelezo ya Abrahams ni kuwa utanzu wa fasihi uliotumia uashiriaji mwanzo ulikuwa ushairi.

Mwanzoni mwa karne ya ishirini Ulaya kazi nyingi za kifasihi zikiwemo mashairi, riwaya na michezo ya kuigiza zilidhihirisha matumizi ya uashiriaji, hususani zile zilizokuwa na mitazamo ya kidini na kijadi. Uashiriaji ulibainika katika matukio, mandhari na matumizi ya lugha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kusadikika* (1951) ya Shaaban Robert mandhari ya nchi inayoelea angani inaweza kuangaliwa kama ishara ya taifa lisilo na msimamo wa haki, sheria na maendeleo thabiti. Nabukonde (2012: 5) akimnukuu T.S. Eliot, anasema kuwa "njia pekee ya mtu kuwasilisha hisia zake kwa umbo la sanaa ni kutafuta kitu au chombo chenye mahusiano kama vile mkusanyiko wa vitu, hali, mfuatano wa matukio, ambao utakuwa fomula ya kuwasilisha hisia hizo." Kutokana na maelezo ya Eliot uashiriaji ni mbinu muhimu katika kuwasilisha hisia za mtunzi na wahusika katika matini bila kuonekana kuibeza hadhira.

Perrine (2014: 173) anaeleza kuwa uashiriaji ni matumizi ya vitu au matukio katika kazi ya kifasihi kiishara. Mbali na vitu na matukio uashiriaji pia unahusu matumizi ya dhana, jina na mandhari kuibua maana za ziada akilini mwa msomaji. Nao akina Frye (1985: 452) wanadai

kuwa uashiriaji ni matumizi ya kipekee ya ishara yanayodhihirisha neno kwa maana yake ya kawaida. Kwa mfano, neno waridi linarejelea ua linaloitwa waridi na dhana inayojitokeza nyuma ya maana, yaani urembo. Kwa sababu hii ua la waridi hutumika kuashiria urembo au umaridadi.

Uashiriaji hulenga kuibua maana mbili, maana ya kawaida ya kiashirii na maana inayohusishwa na kiashirii. Kama anavyodai Cirlot (1962: 14) uashiriaji kiyakinifu ni mfumo unaorejelea mahusiano changamano ambapo uhusiano mwimo ndio unaotawala. Uhusiano huu huunganisha hali halisi na hali dhahania. Hali halisi hurejelea maana ya kawaida inayojulikana na watumizi wa lugha husika ilhali hali dhahania hurejelea maana ya kifasihi inayowakilishwa na ishara. Kimsingi, uashiriaji ni mtindo wa kisanaa wa kutumia vitu, maneno, hali na tukio kwa kusudi la kuwasilisha wazo kidhahania

Uamilifu wa ishara na uashiriaji

Ishara na uashiriaji huwa na umuhimu mkubwa katika ujenzi wa kazi ya kifasihi. Ishara huwa kifaa dokezi cha maana za ziada ili iweze kuibua fikira na hisia changamano bila maelezo marefu. Kwa njia hii ishara huakisi dhima ya itikisadi katika matumizi ya lugha. Sifa hii inadhihirika katika maelezo ya Kennedy na Gioia (2005: 217) wanaposema kuwa ishara hazisimamii tu maana moja bali huweza kuwa kivuli kilichotanda kote. Aidha, uibuaji wa fikira na hisia huzifanya ishara ziwe na uamilifu wa kudokeza hali za kisaikolojia katika kazi za kinathari. Njogu na Chimerah (1999: 34) wanasisitiza kuwa ishara hueleweka katika muktadha wa kitamaduni au wa kimatini. Ufasiri wa ishara kwa maana hii hutegemea ufahamu wa utamaduni wa jamii iliyosawiriwa, itikadi zake na uelewa wa mpangilio wa kiubunifu wa ishara katika kazi yenyewe. Kwa hivyo, uashiriaji husaidia kuweka wazi itikadi na tamaduni za jamii.

Birkerts (1993: 113) anasema kuwa ishara za kifasihi hupata maana kwa kutumiwa kiuradidi katika kazi ya kifasihi au kwa kuwekwa kimakusudi kisanaa katika tukio. Uashiriaji wa kiuradidi unaweza kuwa takriri ya aina fulani katika matini. Ishara ambazo zimetumiwa kiuradidi husaidia kusisitiza ujumbe na vile vile hufanya kazi kama vikale. (Wa Mutiso1996: 19-20)

Uchanganuzi wa aina mbalimbali za ishara zinazojitokeza katika *Nyuso za Mwanamke*

Kwa mujibu wa Frye na wenzake (1985: 453) ishara ni za aina tatu; ishara bia, ishara za kaida na ishara za kifasihi. Ishara bia ni ishara ambazo zinatumia vitu, dhana na hali ambazo watu karibu kila mahali ulimwenguni wanahusiana nazo. Mbatiah (2001: 23) anaeleza ishara za kaida kama ishara ambazo zimepewa maana mahsusi na jamii au utamaduni fulani. Ishara hizi hivyo basi zinajulikana na zinaweza kufasiriwa vizuri na jamii hiyo. Nazo ishara za kifasihi ni ishara ambazo zimebuniwa na mtunzi kutokana na ufahamu wake wa ishara bia na ishara za kaida

pamoja na tajriba yake ya mazingira alimokulia na anamoishi. Ishara za aina hii pia zinaweza kuitwa ishara za kibinafsi kwa vile zinaegemea mtazamo binafsi wa matini fulani.

Ishara bia

Wamitila (2003: 68) anaeleza ishara bia kuwa ni ishara ambazo hutambuliwa na jamii ya walio wengi yaani, jamii ya kimataifa. Ishara bia hueleweka na kutumiwa na jamii ya kimataifa kwani matumizi yake huwa yamepita mipaka ya jamii ndogo ya kabila ama kundi la watu na nchi pia. Ishara za aina hii huweza kufasiriwa na kupewa maana angalau moja na watu wa mataifa mbalimbali. Wamitila anatoa mifano kama vile mto kuonyesha mapito ya maisha, pete kuashiria ndoa, mvua kuashiria neema na milima kuashiria matatizo. Ingawa ishara bia zinawakilisha maana zinazoweza kufahamika na jamii ya kimataifa na utamaduni wake, usuli wake umo katika jamii ambako zilianza kutumiwa kabla ya kuenea kote ulimwenguni.

Uashiriaji kwa ishara bia katika kazi husika unaweza kuangaliwa kuwili. Kuna uashiriaji kimaudhui na uashiriaji kijinsia. Katika uashiriaji kimaudhui ishara bia zimetumiwa kukuza maudhui maalumu katika matini. Kwa upande wake, katika uashiriaji kijinsia ishara bia zimetumiwa kuwakilisha tofauti za kijinsia baina ya wanaume na wanawake katika jamii iliyosawiriwa.

Ishara bia zenye uashiriaji kimaudhui

Ishara bia zimetumika kukuza na kuibua maudhui mbalimbali katika matini. Maudhui haya ni kama vile ya utamaduni na itikadi, mapenzi, uharibifu wa mazingira na umaskini. Katika riwaya ya *Nyuzo za Mwanamke* ishara bia za aina hii ndizo zinazotawala sana. Kwa mfano, kuna kisa cha Faisal, aliyekuwa mchumba wa Bimkubwa, akiwa katika harakati za kumsaka Bimkubwa. Kutokana na tukio hili kunajitokeza mifano ya ishara bia. Tazama kifungu hiki:

> Kunguru weusi peke yao ndio waliokuwa wamestakimu na kutawala hewani, nao, kinyume cha kawaida, anacharaza kelele na fujo pasi na kujali wala kuogopa. […] Haraka kunguru dume na jike walikata hewa. Je, hao ni yeye na Bimkubwa katika mbio za kukimbiana na kutafutana? (*NM*: 14)

Katika mfano huu, kuna ishara zinazowakilishwa na kunguru mweusi, kelele na fujo za kunguru na kunguru dume na jike kupita hewani. Kunguru ni ndege anayenasibishwa na woga kama inavyojitokeza katika tashbihi, mwoga kama kunguru (Wamitila 2004: 60). Kwa upande wake, rangi nyeusi inawakilisha hofu, hatari, mauti na hali isiyojulikana. Kunguru weusi hivyo basi ni ishara ya hali ya hofu na hatari iliyokuwa inamwotea Faisal kwenye mahame hayo. Hatari hii inatokea baadaye Faisal anapodungwa kisu na Bimkubwa na kunusurika kwa tundu la sindano. Nao mlio wa kelele na fujo wa kunguru ni ishara ya uadui na hatari katika mazingira alimokuwamo Faisal. Mohamed (1995: 78) anasema kuwa mlio wa ndege mbaya, anayehusishwa

na mkosi, ni ishara ya uadui na hatari. Baadaye Faisal anadungwa kisu na Bimkubwa aliyemfikiria kuwa mpenzi wake. Ni kawaida pia kwa ndege kuzunguka mahali kuliko na hatari au mnyama mkali kama nyoka wakifanya kelele. Kwa hivyo kelele zao za fujo ziliashiria kuwa ingawa Faisal alijitia ujasiri wa kwenda pale kumsaka Bimkubwa, aliyesakwa hakuwa 'binadamu' tena bali mwehu ambaye angemdhuru badala ya kumkumbatia kwa mapenzi.

Kwa ujumla ishara zinazojitokeza hapo juu zina maana mbili. Kwanza, zinakuza maudhui ya mapenzi baina ya Faisal na Bimkubwa, lakini yaliyokufa. Ingawa Faisal bado anataka kupenda na kupendwa, kwake Bimkubwa mapenzi hayana maana kwa sababu kila mtu amemdhulumu na pia hatamaniki tena. Pili, nafasi ya mapenzi baina yao imechukuliwa na hofu na wasiwasi. Kwa sababu hiyo kuna hatari kwa yule anayesaka. Tatu, uashiriaji kwa ishara hizi unakuza maudhui ya itikadi na utamaduni wa jamii za Kiafrika kuhusu imani za kishirikina.

Mifano mingine ya ishara bia ni mwangaza na giza. Mwangaza huashiria ukweli, ufahamu, usalama au wema (Hall 1996: 91), wakati giza huwa ishara ya uovu, hatari au ujinga (Frye na wenzake 1985: 453). Katika kazi husika mfano ufuatao unakinzana na ukweli huu:

> [...] bado watu wetu wengi wanapoumwa hualiswa ndani siku saba. Hualiswa ndani ya chumba kinchofungwa madirisha kokokoko, ili mwangaza usipenye. […] mwangaza unakuwa sumu na giza dawa. (*NM*: 64)

Katika mfano huu, kuna mkinzano unaotokea kuonyesha mgongano wa utamaduni wa kale na usasa. Kwa mujibu wa Lawrence (2001: 2) mwangaza ni shara ya ahueni na matumaini nayo giza ni ishara ya hofu, hatari na hali ya kukosa matumaini. Katika kifungu hiki ishara hizi mbili zimetumiwa kuonyesha ukinzani kimaana ambapo giza ni ishara ya nafuu na matumaini nayo mwangaza ni ishara ya hofu, hatari na hali ya kukosa matumaini. Ukinzani huu wa kimaana unaonyesha mgongano baina ya itikadi za kale na za kisasa. Kwa wanajadi giza ni bora kuliko mwangaza. Mifano hii inakuza maudhui ya utamaduni na itikadi kwa vile inadokeza utamaduni wa kualishwa watu kama njia ya tiba na imani za jami hii. Aidha, imetumiwa kuaakisi namna sehemu fulani ya jamii, hasa wazee, bado inashikilia tamaduni zilizopitwa na wakati.

Nambari saba ni ishara ya kale inayoashiria uungu na ukamilifu wa Mungu. Lawrence (2001:2) anadai nambari saba kama ishara ya kale imeundwa kutokana na nambari tatu ambayo ni ishara ya uungu na nambari nne inayoashiria ukamilifu wa binadamu. Kwa mfano, kuna siku saba za fungate, siku saba za uganga, siku saba za kualikwa na siku saba za Mungu (*NM*: 63). Ingawa ishara hii usuli wake ni wa kidini, hasa Wakristo na Waislamu, kwa sasa inatumika katika jamii na tamaduni mbalimbali za ulimwengu. Matumizi ya ishara hii ina maana mbili. Kwanza, matatizo yanayowakumba wanawake, kwa mtazamo wa itikadi za kijadi, yana uvumbuzi kwa kuzingatia itikadi zizo hizo. Pili, itikadi za kijadi bado zina nguvu na ndizo nyenzo kuu ya

kumgandamiza mwanamke katika jamii husika. Kwa maana hii ishara hii inakuza maudhui ya nafasi ya mwanamke mbali na ya utamaduni na itikadi.

Ishara zinazorejelea mazingira na mandhari ya nchi zimetumika pia. Nchi au ardhi ndiyo asili ya utajiri na maliasili. Kwa hivyo, upungufu au dosari zozote katika maumbile ya nchi ni ishara ya ufukara au uharibifu. Ugunduzi wa Nana, ambaye ni mhusika mkuu, unadokeza haya:

> Aridhi ilionekana kwa ujumla tasa kabisa. […] Miti pekee iliyotamalaki pande hizi ni mikayaya iliyojitokeza kwa vituwe hapa na pale, vituwe vistahamilijoto la jangwa. […] Mchwa, ni viumbe pekee vilivyojua kuishi na kutawala katika mazingira haya nje na ndani ya skyscrappers zao. (*NM*: 89)

Kumetajwa aridhi tasa, mikayaya na mchwa. Ardhi tasa inarejelea jangwa au nyika ambapo ni mahali palipo na mvua kidogo au pasipo na mvua kabisa. Jangwa ni ishara ya ukiwa na umaskini kama anavyotaja Lawrence (2001: 3). Nayo mikayaya ni ishara ya uvumilivu na ukakamavu.

Uashiriaji kwa ishara hizi unakuza maudhui ya umaskini na uharibifu wa mazingira. Zinaonyesha kuwa watu wanaokaa katika mazingira haya yaliyojaa umaskini wanahitaji ukakamavu na uvumilivu ili wakabiliane na hali hii ngumu. Mchwa ni wadudu wanaojulikana kwa ushrikiano na bidii. Kwa hivyo, mchwa ni ishara ya bidii na ushirikiano (Lawrence 2001:4). Ushirikiano baina ya wanajamii unahitajika ili kuyatatua matatizo yao hususani uharibifu wa mazingira na upungufu wa rasilimali. Ishara hizi zina maana kuwa binadamu hawezi kufaulu katika ulimwengu uliojaa ufukara na taabu bila ya bidii na utangamano usiokuwa na ubaguzi. Hii ndiyo itikadi ya mhusika mkuu, Nana.

Ishara zinazorejelea wadudu, mimea na hali ya anga, ambazo nyinginezo ni ishara bia, pia zimetumiwa. Uashiriaji huu umewiana vizuri na mandhari alimokuwa Faisal, ya porini. Uashiriaji wa kitaswira unaojitokeza hapa chini una dhima ya kukuza maudhui ya mapenzi.

> Wakati huu ndipo Faisal alipogutuka kutokana na ile ndoto ya maisha yake ya wakati uliopita. Mbele yake aliona mvua ya vipepeo ikinyesha. Vipepeo vya kila aina, vya kila sanaa ya mpangilio wa rangi na kila vimo na wasifu. […] Mabonge ya mawingu rangi ya kijivu yanafunika samawati juu ya mbingu […] Jua likaanza kuchungulia na anga likaangusha chini miale ya fedha. […] Maua mbalimbali yakapata nafasi ya *kujisasambua* rangi zao na kualika ndege na vipepeo kufyonza viriba vyao vya asali. (*NM*: 251)

Kipepeo ni mdudu mrembo na mtulivu. Kwa kawaida taswira ya vipepeo wengi wanaopaa angani hupendeza. Hall (1996: 54) anadai kuwa kipepeo ni ishara ya uhai, upendo na ulimbwende. Mfumuko wa vipepeo wengi hivyo basi ni ishara ya kunawiri kwa mapenzi yaliyokuwepo kati ya Faisal na Bimkubwa. Hata hivyo, mapenzi haya yaliyonawiri yanafunikwa na mawingu. Mawingu kwa mujibu wa Hall (1996: 75) ni ishara ya hali isiyojulikana. Katika muktadha wa kazi husika mapenzi baina ya Bimkubwa na Faisal yalipingwa na babake Nana lakini kuhama kwa Faisal hadi Abu Dhabi kutokana na vita vya mapinduzi ni hali ambayo haikutarajiwa kabisa.

ISHARA NA UASHIRIAJI KAMA NYENZO YA MTINDO, MAANA NA KIWAKILISHI CHA ITIKADI KATIKA RIWAYA YA *NYUSO ZA MWANAMKE*

Hali hii ilimtoa Faisal machoni mwa Bimkubwa na kusababisha babake kumwoza kwa Bwana Hila kwa nguvu.

Katika kifungu hiki "jua linalochungulia" linarejelea hali ya Faisal kuendelea kutamani mapenzi baina yake na Bimkubwa yanawiri hata wakati Bimkubwa ameozwa kwa bwana mwingine. Ua huwa zuri kama Bimkubwa alivyokuwa mrembo katika ujana wake. Baadaye anafyonzwa na wanaume na kunyauka kama linavyonyauka ua baada ya kufyonzwa na ndege na vipepeo. Maana yake ni kuwa mapenzi kati ya Bimkubwa na Faisal yalikuwa yamenawiri sana lakini kwa sasa hayapo na Bimkubwa ametumiwa vibaya na ulimwengu na kuachwa gofu tu. Maudhui ya ukombozi wa mwanamke kutokana na dhuluma na udhalilishaji yanadokezwa hapa. Aidha, uashiriaji huu unaonyesha imani ya Faisal ya kuendeleza mapenzi baina yake na Bimkubwa.

Wimbo alioutunga Faisal kuomboleza kunyimwa Bimkubwa pia unatumia kipepeo kama ishara ya mwanamke mrembo, anayechukuliwa kuwa ni Bimkubwa.

Kipepeo
Huruka na kunijia — Na kutua mikononi
Vyema anavyonukia — Na pambo linalo shani
Huja kunitembelea — Kipepeo wa moyoni
Kiitikio:-
Kipepeo wende na kurudi — Mpaka tupojaliwa
Itapotimu miadi — Roho zetu zitapowa (*NM*: 252)

Katika wimbo huu Faisal anamrejelea Bimkubwa kama kipepeo. Kama tulivyotaja hapo juu kipepeo ni ishara ya mapenzi. Katika wimbo huu kipepeo anarejelea mapenzi ya dhati ya Faisal kwa Bimkubwa.

Mwangaza na ua ni ishara nyingine ambazo zimetumiwa katika kazi hii. Wakati Nana anapomwalika Amour anawasha mshumaa na kuweka pale ua la waridi lenye harufu nzuri kama inavyojitokeza katika dondoo hii.

> Muda ukapita. Mshumaa juu ya meza ukaendelea kupiga *vipezi* na kucheza *danedane*. Ua la waridi lililokuwa likifyonza maji ndani ya bakuli la maua lilihanikiza harufu tamu. (*NM*: 264)

Hall anadai kuwa mshumaa uliowashwa ni ishara ya nuru ya imani (1996: 57). Kwa upande wake nuru ni ishara ya matumaini, ukweli na usalama. Hii ni ishara bia ambayo ni dhahiri inayojitokeza katika mandhari ya nyumba ya Nana kuonyesha hali ya kuwa na imani na matumaini ya mapenzi baina yao kunawiri. Nalo ua la waridi ni ishara ya ulimbwende. Kwa maana hii, ua la waridi na harufu inayoenea ni ishara ya mapenzi ya dhati yaliyokuwepo kati yao

ambayo hayakuwa na dalili yoyote ya kukatika. Matumizi ya ishara hii si ya kisadfa bali yamedhamiriwa na mtunzi kutuonyesha namna wawili hawa walivyopendana na wakati huo huo kukuza maudhui ya mapenzi. Suala la mapenzi limesisitizwa sana kwa matumizi ya ishara kuonyesha umuhimu wake katika maisha ya binadamu na matini kwa ujumla.

Ishara bia za jinsia

Ishara bia za jinsia ni ishara zinazorejelea tofauti za kijinsia baina ya wanaume na wanawake. Ishara hizi kama nitakapoeleza hivi punde zina mwelekeo mkubwa wa tofauti za kimaumbile baina ya wanaume na wanawake kama anavyoeleza Freud katika kitabu chake, *The Interpretation of Dreams* (1900): yaani "Ufasiri wa Ndoto." Aidha, ishara hizi hutokana na taswira za vifaa na maumbile asilia kama vile mwezi na jua. Freud anadai kuwa ndoto huwasilishwa kwa ishara ambazo kudhihirisha uana, yaani hali ya kike na kiume (1900: 351-353). Kulingana na Freud ishara zinazowakilisha hali za kike zina mpanuko au mfunuko kama ua na ziwa nazo ishara zinazowakilisha jinsia ya kiume zimesimama kama penseli, kalamu au mkuki, yaani zenye ukali au zilizochongoka. Kutokana na utafiti wake kuhusu ufasiri wa ndoto alibainisha ishara zifuatavyo;

Ishara za kiume	Ishara za kike
kijiti	boksi
mwavuli	kabati
kisu	chumba
ufunguo	kufuli
chuma	ubao
jua	mwezi

Wakati wa Freud ishara hizi zilipotokea katika ndoto ufasiri wa ndoto hizo ulitegemea ufasiri wa ishara hizi. Ingawa ishara hizi zina mwelekeo mkubwa wa tofauti za kimaumbile na unyanyapaa wa kijinsia, ufasiri wake katika matini za kifasihi unaweza kusaidia kupata ujumbe wa msanii kikamilifu. Katika *Nyuso za Mwanamke* kuna matumizi ya ishara zinazorejelea hali za kike na kiume. Kuna matumizi ya ishara inayorejelea mwezi. Kama alivyodai Freud mwezi ni ishara ya jinsia ya kike kwa sababu ina mpanuko. Nana alipotazama mwezi aliona kijana ameketi juu yake akimpungia mkono. Baadaye akajiwa na wimbo ufuatao:

Ewe Mwezi	
Unapochomoza	Na uzuri wako
Unanipumbaza	Kwa kicheko chako
Kuwa n'naweza	N'ngekuja kwako

ISHARA NA UASHIRIAJI KAMA NYENZO YA MTINDO, MAANA NA KIWAKILISHI CHA ITIKADI KATIKA RIWAYA YA *NYUSO ZA MWANAMKE*

Kiitikio:-
Ewe mwezi ewe azizi Nipe mbawa nirukiye
Ewe mwezi ewe mpenzi Nipe ngazi nipandiye
Nikiona sura yako Akili zinaniruka
Lakini umbali uliko Vipi huko nitafika?
Nataka shauri lako Kama nawe wanitaka
Kiitikio:-
Ewe mwezi ewe azizi Nipe mbawa nirukiye
Ewe mwezi ewe mpenzi Nipe ngazi nipandiye (*NM*: 228)

Kwa mujibu wa Freud mwezi ni ishara ya mwanamke anayependeza na kuvutia. Naye Hall (1996: 213) anaeleza kuwa mwezi ni ishara ya usafi na ubikira. Kwa maana hii mwezi katika wimbo huu ni ishara ya mwanamke safi na ambaye hajaingiliwa kingono. Mwanamke huyu ni mhusika Nana aliyekuwa mrembo ajabu. Juu ya mwezi kuna kijana mwanamume aliyeketi. Kuketi huku ni ishara ya Nana kutawalia na kijana, Amour, kwa mapenzi. Kama anavyodai Lyman (2000: 6) ishara hufasiriwa kwa kutegemea mahusiano yaliyopo kati ya kiashirii na kiashiriwa. Katika mfano huu, kuna uhusiano mkubwa kati ya wimbo huu, mwezi na hali halisi iliyopo ya mapenzi yanayonawiri kati ya Nana na Amour. Ingawa ishara hizi zimeainishwa kama za kijinsia zina uamilifu wa kudokeza maudhui ya mapenzi na zimewekwa hapa kimakusudi katika msuko wa kazi hii ili kuonyesha jinsi Nana na Amour walivyotawaliwa na mapenzi baina yao.

Katika mfano tuliotoa hapo juu kuna ishara za kijinsia ambazo zimetumika. Kumetumika maua, vipepeo na ndege. Ua ambalo lina mtanuko ni ishara ya mwanamke kama anavyoeleza Freud. Nao vipepeo na ndege katika tendo lao la kufyonza viriba vya maua ni ishara za wanaume. Sababu ya kuchukulia ndege na vipepeo kuwa ishara ya wanaume katika muktadha huu ni kile kitendo chao cha kufyonza asali kwa vidonda vyao vilivyochongoka kama alivyodai Freud. Tendo lao linaashiria namna wanaume wanavyowatumia wanawake vibaya na kuwadhalilisha. Bimkubwa alitumiwa hivyo hadi akawa mwendawazimu.

Ishara bia ndizo zinazojitokeza sana. Matumizi haya yanawiana na suala kuu linalokuzwa katika matini ambalo ni udhalilishaji wa mwanamke na ukombozi wake. Suala hili halijaathiri jamii fulani tu bali ulimwengu mzima zikiwemo jamii za nchi zilizostaarabika zaidi. Matumizi haya yanaakisi namna suala hili lilivyo bia na ukombozi wake unahitaji juhudi za walimwengu wote.

Ishara za kaida

Kunazo ishara za kaida ambazo zimejikita katika jamii fulani tu na hazivuki mipaka ya kabila, yaani kundi la watu au taifa. Kwa mfano, katika jamii ya Waluhya wa magharibi mwa Kenya, mbwa mweusi ni ishara ya mkosi fulani na nyama nyingi katika ndoto ni ishara ya mauti. Inafaa ikumbukwe kuwa ishara bia na za kaida zinawakilisha itikadi na utamaduni wa jamii asilia ambapo zilibuniwa mwanzo.

Baadhi ya ishara za kaida zinaweza kuwa za kijadi kwa kuwa zina historia ndefu katika jamii husika na hujitokeza kama sehemu ya utamaduni wake. Ishara za aina hii pia zinajitokeza katika kazi hii. Katika mfano huu hapa chini kuna milio ya ndege na wanyama ambayo katika jamii za kijadi za Kiafrika huchukuliwa kuonyesha kutokea kwa tukio baya au mkosi.

> Ilibidi hatimaye sikio lake la ndani lifumbuke aliposikia sauti ya bundi *ikiritibua* utulivu alioutaka uendelee usiku huo kucha. "Hoooood!" Bundi alilia. Tena zikafuata kwerezo za popo kama msumeno uliokata Chuma. "Kweeerrrch!" Baadaye mpazo wa sauti ya punda isiyoweza kuelezeka "Haaa-mb, haaa-mb." Tena ghafla, kipepo, vuuuu, kikajiingiza ndani pasi na kukaribishwa. Halafu kimya, kimya kilichonata ute mweusi wa usiku. (*NM*: 229)

Milio isiyo ya kawaida ya wanyama katika jamii nyingi za Waafrika huashiria mkosi wa aina fulani au tukio baya litakalotokea. Mlio wa bundi karibu na makazi ya watu ni ishara ya kifo au mkosi katika boma husika. Kwa sababu hii ndege hawa wanapolia karibu na boma hufukuzwa. Kwa hivyo bundi anahusishwa na mkosi katika jamii nyingi za Afrika Mashariki tofauti na jamii ya Kiyunani ambako ni ishara ya hekima (Hall 1996: 231). Milio hii inatokea karibu na makazi ya Nana ambayo baadaye yanakumbwa na mkosi wa kuchomeka kwa nyumba ya Nana wakati wa harusi. Utulivu unaoshuhudiwa baada ya milio hii ni ishara ya utulivu anaopata Nana katika maisha yake baada ya hamkani nyingi. Ishara hizi ni sehemu ya itikadi za kishirikina za jamii husika. Vilevile, ishara hizi zinaonyesha kuwa ingawa watu wa jamii hii wameelimika bado wanashikilia itikadi za kishirikina. Ishara hizi zimetumika katika matini kukuza maudhui ya utamaduni na itikadi za jamii.

Ishara za kifasihi

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001: 23) ishara za kifasihi ni ishara ambazo zimebuniwa na mtunzi kuwakilisha maana fulani na wala hazirejelei utamaduni au jamii fulani. Ishara za aina hii zimejikita katika msuko wa kazi kutegemea ubunifu wa mtunzi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kaburi Bila Msalaba* (1969) ya Peter Kareithi, kaburi bila msalaba ni ishara ya vifo vingi vya Waafrika katika vita vya Mau Mau ambao hawakupewa maziko yoyote ya maana. Katika kazi husika kuna ishara ambazo zimebuniwa na mtunzi ili kuwasilisha maana fulani za kifasihi na kijamii. Mfano wa ishara ya kifasihi unajitokeza hapa chini.

> […] alimwona pugi juu ya mpendapendapo ambapo alianza kulia kwa sauti ya ajabu. Ilikuwa si sauti ya huzuni wala furaha. Sauti ya mkato tu – isiyotiwa chumvi wala sukari, sikwambii limau. […] Mlio wa leo lakini haukufanana na mlio wowote aliowahi kuusikia. (*NM*: 246)

Mlio wa pugi wa ajabu ni mlio usio wa kawaida. Kwa hivyo, ni ishara ya mabadiliko katika ulimwengu wa hali ya maisha ya Faisal kuendelea kutulia ingawa haiwezi kusemwa kuwa imeboreka. Mabadiliko yanayotokea ni ya Nana kuchumbiwa na Amour, yaani mwana kumpokonya baba mwandani wake. Jambo hili linamfanya Faisal kuhamia Morishas bila kutoa habari ya awali kwa yeyote. Hii inakuwa afueni kwake na biniye. Kuingizwa kwa ishara hizi kunachangia kukuza msuko wa matini na kuwa utabiri wa yatakayotokea.

Kama alipotaja Birkerts (1993: 113) ishara za kifasihi hupata maana kwa kutumiwa kiuradidi au kwa kuwekwa kimakusudi kisanaa katika tukio. Kuwekwa huku kimaksudi kunarejelea hali ya mtunzi kutumia ishara fulani kwa maksudi maalum. Ishara zinapotumiwa hivi huwa na uwezo mkubwa kubainisha maana kwa nguvu sana. Aidha, uradidi huu husaidia kudokeza na kusisitiza ujumbe katika matini. Kuna nambari saba ambayo imetumiwa hapa tena katika muktadha tofauti.

> Je, kulikuwa na ishara njema kwangu zilizotoka kwenye uso huu wa maumbile? Baadaye madege ya pwani yalikuja kunizunguka mara saba. Yalinizunguka kwa kwenzi juu ya kichwa changu kama vile *wakinizingua.* (*NM*: 129)

Nambari saba ni motifu inayojitokeza katika kazi nyingi za kifasihi hasa zenye mafungamano na Ukristo na Uislamu. Nambari saba ni ishara ya kale inayorejelea uungu na ukamilifu wa Mungu au kilele cha ufanisi kama tulipotaja hapo juu. Kwa maana hii tendo la madege kumzunguka Nana mara saba ni ishara ya Nana kufikia kilele cha ufanisi katika maisha yake. Baada ya muda usiokuwa mrefu tunamwona Nana akifanikiwa kupata hundi aliyowekewa na mama yake iliyomsaidia kuanzisha biashara kubwa sana. Hali hiyo pia ni ishara ambayo imetumiwa kama utabiri wa kuboreka kwa maisha ya Nana baadaye. Ni dhihirisho la nguvu kama za kiungu katika maisha ya mhusika huyu za kuyaona mambo mema kwa mbali kabla hayajatokea.

Ishara za kifasihi kama mbinu ya kihusika

Ishara za kibinafsi pia zimejitokeza kama mbinu ya kuwakuza wahusika. Matumizi ya aina hii ya ishara huitwa uashiriaji jina (Perrine 2014: 197). Mtunzi amefanya hivi kwa kudokeza sura aina mbili kuu za wahusika wa kike. Kwa upande mmoja kuna uso wa mwanamke ambaye amedhalilishwa na kudhulumiwa na jamii. Katika uso huu kuna nyuso nne za wanawake: uso wa watoto wa kike wanaofariki wakiwa wachanga, uso wa wanawali wanabakwa na kuozwa kwa lazima, uso wa wake wanaodhulumiwa katika ndoa na uso wa wajane wanaonyima urithi wao (Mohamed 2010: 183). Kwa upande mwingine kuna uso wa mwanamke aliyeamua kuasi mila na desturi za kitamaduni na kidini ili ajikomboe.

Nyuso hizi mbili ni kinzani kwa vile moja ni hasi na nyingine ni chanya. Uso hasi unawakilishwa na Bimkubwa na uso chanya unawakilishwa na Nana. Nana amesawiriwa kama ishara ya ukombozi wa mwanamke kwa namna anavyoongoza juhudi za kujikomboa na kuwakomboa wanawake wengine. Kwanza, anapinga kuengwaengwa na baba yake kama yai na baadaye anatoroka ili awe huru kujiamulia mambo yake. Aidha, anakataa msaada wa pesa kutoka kwa Faisal kama mtaji wa kuanzisha bendi ya taarabu. Alipofanikiwa alipanga mikakati ya kuwaelimisha na kuwafadhili wanawake waliodhulumiwa. Uso huo wa Nana unajitokeza kati ya nyuso nyingi hasi kwa vile si wanawake wengi wanaothubutu kujitolea kuasi itikadi zao na kupigania maslahi ya wenzao. Kwa njia hii Nana amesawiriwa kama mhusika wa kimapinduzi katika ukombozi wa wanawake. Aidha, Nana kama kijana ametumika kuonyesha umuhimu wa vijana kuongoza juhudi za kuleta mabadiliko ya kijinsia. Maudhui ya ukombozi wa mwanamke yamekuzwa kwa uashiriaji huu.

Bimkubwa naye ni ishara ya kilele cha udhalilishwaji wa wanawake katika jamii hii kwa jinsi anavyokumbwa na mateso ya kila aina hadi akawa mwendawazimu na akajinyonga. Kwanza, anaozwa kwa Bwana Fadhila kwa nguvu ingawa alikuwa amechumbiwa na Faisal. Pili, ananyimwa uhuru na mume wake wa kwanza hali iliyomfanya atoroke. Baadaye anaolewa mara mbili na ndoa zote zilikuwa za kitumwa kiasi cha kumfanya mwendawazimu. Uashiriaji huu unakuza maudhui ya dhuluma na udhalilishaji wa wanawake katika jamii.

Naye Faisal ni ishara ya mabadiliko ya kijamii katika masuala ya kijinsia katika jamii ya utandawazi. Kwanza, yuko tayari kuwasaidia wanawake wanaodhalilishwa kama Nana. Pili, anaamini kuwa vijana wanapaswa kujichagulia wenzi wa kuoa. Hali hii ni dalili ya mabadiliko yanayoingia katika jamii nyingi za Kiafrika ambapo wanaume wanaanza kuona kuwa kuna usawa na kwa hivyo wanawake hawapaswi kudhalilishwa na kudhulumiwa.

Hitimisho

Nimejadili aina tatu za ishara, ishara bia, ishara za kaida na ishara za kifasihi. Ishara zinazojitokeza kwa wingi ni ishara bia. Uashiriaji huu umefaulu kudokeza maana mbalimbali za kifasihi, kukuza maudhui na kusawiri wahusika. Masuala makuu yaliyojitokeza ni kama mapenzi, itikadi na utamaduni, dhuluma dhidi ya wanawake, umaskini, uharibifu wa mazingira na haki za wanawake ambalo ni suala la kimataifa linaloathiri wanawake wote. Ishara za kifasihii pia zimetumiwa kuonyesha ubunifu wa mwandishi na zimewekwa katika matini kiufundi. Ishara za kaida ni chache kuonyesha hali halisi ya ulimwengu wa utandawazi ambapo linalotendeka katika pembe moja ya ulimwengu ni rahisi kufahamika na pembe nyingine ya ulimwengu. Aidha, wahusika pia wamesawiriwa kiishara kuonyesha uhusika wa kipekee katika kazi hii. Uhusika huu wa kiishara ni mchango mkubwa katika kukua kiutanzu kwa riwaya ya Kiswahili.

ISHARA NA UASHIRIAJI KAMA NYENZO YA MTINDO, MAANA NA KIWAKILISHI CHA ITIKADI KATIKA RIWAYA YA *NYUSO ZA MWANAMKE*

Mwandishi amefaulu sana kutumia ishara kwa vile zimewiana sana na matukio na mandhari yaliyosawiriwa katika kazi yake. Ishara hizi zimefaulu sana kuwasilisha maana, kukuza maudhui na kuwakilisha itikadi au utamaduni wa jamii husika. Uchanganuzi zaidi unaweza kufanywa kuangazia namna ishara zinavyochangia kukuza ploti, mandhari na mtazamo wa mtunzi katika matini. Uashiriaji jina pia unaweza kuchunguzwa kubainisha namna unavyojitokeza katika riwaya mpya ya Kiswahili.

Marejeleo

Abrams, Meyer H. 1971. *A Glossary of Literary Terms.* New York: Holt, Rinehart & Winston.

Baudelaire, Charles. 1857. *Les Fleures du Mal*. Paris: Auguste Poulet-Malassis.

Bin Nasir, Sayyid Abdalla bin Ali. 1977. *Al-Inikishafi. Catechism of a Soul*. Nairobi, Kampala & Dar es Salaam: East African literature Bureau.

Birkerts, Sven. 1993. "Symbolism," *Literature: The Evolving World.* Boston: Allyn and Bacon.

Cirlot, Juan E. 1962. *A Dictionary of Symbols.* London: Routledge & Kegan Paul.

DiYanni, Robert. 1998. *Literature: Reading Fiction, Poetry and Essay*. (4) Boston: MacGraw Hill.

Freud, Sigmund. 1900 *The Interpretation of Dreams.* London: Hogarth Press.

Frye, Northrop, Warner B. Sheridan & George B. Perkins. 1985. *The Harper Handbook of Literature*. New York: Harper Collins.

Hall, James. 1996. *Dictionary of Subjects and Symbols in Art* (Revised edition). London: John Murray.

Kareithi, Peter M. 1969. *Kaburi Bila Msalaba*. Nairobi: East African Publishing House.

Kennedy, X. Joseph & Gioia, Dana (Eds.) 2005. *Literature: An Introduction to Fiction, Poetry and Drama*. New York: Longman.

Lawrence, Lisa. 2001. *Archetypes and Symbolss.* Jenks. Makala ambayo hayajachapishwa.

Lyman, Stanford M. 2000. "Symbolism." *Literary Concepts*. Makala ambayo hayajachapishwa. University of Virginia.

Mbatiah, Mwenda. 2001. *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks.

Meyer, Michael. 2002. *The Bedford Introduction to Literature.* London: Bedford and Martins.

Mohamed, Said A. 1995. *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, Said A. 2010. *Nyuso za Mwanamke.* Nairobi: Longhorn.

Nabukonde, Lucy L. 2012. *Symbolism in Ugandan Poetry.* Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, Kimani & Chimerah, Rocha M. 1999. *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Paris, Bernard J. 1974. *A Psychological Approach to Fiction.* Bloomington: Indiana University Press.

Perrine, Laurence. 2014. *Literature: Structure, Sound, Sense*. Boston: Wadsworth

Robert, Shaaban. 1951. *Kusadikika*. London: Nelson.

Snowden, Ruth. 2006. *Freud – the Key Ideas*. (*Teach Yourself* series). London: Hodder Education.

Wa Mutiso, Kineene. 1996. *Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida ya Burudai*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Wamitila, Kyallo W. 2003. *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus.

Wamitila, Kyallo W. 2004. Kamusi ya Tashbihi, Vitendawili, Milio na Mishangao. Nairobi: Longhorn.